

## **TAASISI 12 ZA SERIKALI ZAKAGULIWA NA TUME YA UTUMISHI WA UMMA**

### **Imetolewa na Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma.**

Tume ya Utumishi wa Umma imekagua Taasisi 12 za serikali ili kuona hali ya uzingatiaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002 kama ilivyorekebishwa na Sheria Na. 18 ya mwaka 2007, Kanuni na Taratibu zake za mwaka 2003.

Ukaguzi huo umeanza 25/1/2010 na unatarajiwa kukamilika 29/1/2010.

Taasisi za serikali zilizokaguliwa ni Halmashauri ya Wilaya ya Hai, Sekretarieti ya Mkoa wa Kilimanjaro, Halmashauri ya Jiji la Mbeya, Halmashauri ya Wilaya ya Magu, Halmashauri ya Wilaya ya Masasi na Lindi. Aidha, Taasisi nyingine ni Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro, Halmashauri ya Wilaya ya Lushoto, Halmashauri ya Ngara, Halmashauri ya Mji wa Babati, Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga na Halmashauri ya Wilaya ya Karagwe.

Taasisi hizo zimekaguliwa katika maeneo mbalimbali ya kitumishi, ikiwamo masuala ya ajira na nidhamu, ili kuona kama taasisi hizo zimeongeza au la uzingatiaji wa sheria ya Utumishi Na. 8 ya mwaka 2002, kanuni na taratibu zake za mwaka 2003.

Ukaguzi unaofanywa na Tume ni wa kisheria, ambapo kuna ukaguzi wa kawaida na maalumu. Tume hufanya ukaguzi maalumu iwapo imepata taarifa kwamba Taasisi ya Serikali au baadhi ya taasisi za serikali haziendeshi masuala ya Rasilimali watu kwa mujibu wa sheria ya Utumishi wa Umma Na. 8 ya mwaka 2002. Aidha, ukaguzi wa kawaida ni ukaguzi ambao Tume hupanga katika utaratibu wake wa kawaida wa kukagua taasisi za serikali kila mwaka.

Tangu Tume ya Utumishi wa Umma ianze kazi rasmi mwaka 2004, uzingatiaji wa sheria ya Utumishi Na. 8 ya mwaka 2002, kanuni na taratibu zake imepanda kutoka 52% kwa mwaka 2005/2006 hadi kufikia 70% kwa mwaka 2007/08. Kuongezeka kwa uzingatiaji huo

kumetokana na kuongezeka kwa elimu inayotolewa na Tume kwa njia mbalimbali, ikiwamo kufanya mikutano na wadau, kuandaa na kusambaza miongozo kwa wadau mbalimbali.

Ukaguzi unaomalizika leo utaendelea tena katika awamu ya II baada ya tume kupanga kazi hiyo.

Katika kipindi hiki tume imepanga kukagua jumla ya taasisi 27 za serikali. Tayari imeshakagua taasisi nyingine za serikali ambazo ni pamoja na Wizara na Idara zinazojitegemea za serikali.

Iwapo una maoni/maswali tafadhali tuandikie:

**Katibu,  
Ofisi ya Rais,  
Tume ya Utumishi wa Umma,  
S.L.P. 9143,  
Dar es Salaam.**